



Kiswahili Paper 3

Form 3

MARCH EXAMINATION 2021

1 hr. 30 min

Additional Materials:

- Soft clean eraser
- Soft pencil (type B or HB recommended)

Read these instructions first

This paper contains 4 sections. Answer all questions in the spaces provided.

Do **not** use staples, paper clips, and glue or correction fluid.

Any rough working should be done in the rough work booklet provided.

NAME:

DATE:

SCORE:

TOTAL MARKS:

[Turn over]

SEHEMU A:TAMTHILIA

KIGOGO: PAULINE KEA

Uliona nini kwa huyo zebe wako? Eti mapenzi!

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (A1.4)

b) Andika mbinu mbili za lugha zinazojitokeza kwenye dondoo hili. (A1.4)

c) Taja hulka/sifa za mnenaji zinazojitokeza kwenye dondoo hili. (A1.2)

d) kwa kurejelea Tamthilia nzima ya Kigogo,Elezamaudhui yoyote manne yanayoendelezwa na mwandishi. (A1. 10)

SEHEMU B: FASIHI SIMULIZI

- a) Taja Tanzu zozote Sita za Fasihi simulizi. (Al 6)
- b) Tofautisha Kati ya Fasihi Simulizi na Fasihi Andishi. (Al 14)

SEHEMU C: HADITHI FUPI**TUMBO LISILOSHIBA NA HADITHI ZINGINE****KENNA WASIKE: MAPENZI YA KIFAUONGO**

...kabwela Kama mimi nina faida gani...?

- a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (Al 4)
- b) Taja mbinu mbili za lugha zinazojitokeza kwenye dondoo hili. (Al 4)
- c) Taja na ueleze kimuhtasari maudhui yoyote manne yanayojitokeza katika hadithi ya "Mapenzi Ya Kifaurongo." (Al 12)
2. Taja na ueleze sifa zozote TATU za wahusika hawa. (Alama 20)

Dennis

Penina

SEHEMU D: USHAIRI

Soma shairi lifuatalo kwa makini Kisha ujibu MASWALI yanayofuata. (Alama 20)

1. Ukitazama dunia, umbo lake huarifu,
Kuwa imeandaliwa, wageni watukufu,
Tayari kuwapokea, na mambo sufufu,
Ndani yake yamejaa, viumbe kuwanadhifu.

2. Umbile huonyesha, namna ilivyotimu,
Yangoja kukaribishwa, katika mastakimu,
Yenye kila tamasha, machungu na matamu,
Maisha yanapokwisha, huiacha inadumu.

3. Ajae ardhi hii, kutoka katika mimba,
Mzizini au yai, au katika kitumba,
Milki hakinai, ya mali wala mashamba,
Mwisho wa uhai, kaburi lake jemamba.

4. Halii choyo kaburi, mtu uzima ukisha,

La upana shubiri, urefu pima yatosha,
 Wala hadai fahari, tena hujifaharisha,
 Akiwa hai fikiri, anavyopenda tamasha.

5. Yalipo maziara, masikani ya maiti,
 Huonyesha ishara, na pengine tofauti,
 Dhaifu na bora, hawagombi hawateti,
 Wazima kila mara, Pato linawasalitia.
6. Mtu hashibi pato, hili huonyesha nini?
 Laonyesha kama pito, kuwa yumo safarini,
 Enda kuitika wito, bora usio kifani,
 Ambao kila mtoto, wa Adam hutamani.
7. Yumo katika safari, kila mwanadamu,
 Haraka au usiri, kwenda imelazimu,
 Epusha roho kahari, yake na Jahanamu,
 Iwe katika fahari, mwili ukiwa kuzimu.

Maswali:

- (a) Pendekeza kichwa cha shairi hili. (alama 2)
- (b) Mshairi amevitaja vitu aina ngapi vyenye uhai? Vitaje. (alama 4)

- (c) Andika ubeti wa tatu kwa lugha nathari. (alama 5)
- (d) Eleza vina na mizani katika shairi hili. (alama 3)
- (e) Eleza ujumbe wa mshororo:
"Halii choyo kaburi, mtu uzima ukishe." (alama 2)
- (f) Onyesha vile uhuru wa kishairi ulivyotumiwa. (alama 4)